

ASb
approved



Kiswahili

Anansi mvivu

Brigid Simiyu

Wiehan de Jager

Anansi ni buibui mvivu.



Anapenda chakula,
lakini hapiki kwani
ni mvivu.

Anansi anamtembelea Sungura.

Anaomba wale mboga pamoja.



"Nisaidie
kukoroga,"
Sungura anasema.

Anansi hataki, ni
mvivu.

"Nitarudi baadaye," Anansi anasema.



Anafunga utando
mguuni na kwenye
chungu cha
Sungura.

"Vuta utando mboga zitakapoiva," Anansi
anasema.



"Kima, naomba
nile maharage
nanyi?"

"Tusaidie kufanya
kazi."

"Nitarudi," Anansi anasema.

Anafunga utando zaidi.




"Ngiri, tule viazi
pamoja?"

"Nisaidie
kuvitayarisha,"
Ngiri anamjibu.

"Nitarudi," Anansi anasema.


Anafunga utando zaidi.



Hatimaye, kila
mguu wa Anansi
umefungwa
kwenye chungu.

Anansi anavutwa kwenye mguu wa 2.

Halafu mguu wa 3.



Miguu yote 8
inavutwa!

"Acheni kuvuta!"
Anansi analia.

Hakuna anayemsikia Anansi.

Utando unakatika mmoja mmoja.



Ndiyo sababu
buibui wote wana
miguu mirefu
myembamba.

You are free to download, copy, translate or adapt this story and use the illustrations as long as you attribute in the following way:

Anansi mvivu

Author - Ghanaian folktale

Translation - Brigid Simiyu

Illustration - Wiehan de Jager

Language - Kiswahili

Level - First words

© African Storybook Initiative 2014

Creative Commons: Attribution 4.0

Source www.africanstorybook.org

